USAID
KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI

# MIFUMO YETU

## Jarida la Mifumo ya TEHAMA ya TAMISEMI

TOLEO NA. 11 Novemba 2019 — Januari 2019



TAMISEMI
KIDIJITALI
TUMEIFIKIA MIKOA 26, HALMASHAURI 185 TANZANIA NZIMA

*Jarida hili limeandaliwa kwa ushirikiano kati ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3).*

*“ Jarida hili limefanikishwa kwa msaada wa watu wa Marekani kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), chini ya Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3). Ofisi ya Rais -TAMISEMI ndiyo itakayowajibika na matokeo ya kazi hii. Jarida hili ni maoni ya*

*Ofisi ya Rais-TAMISEMI, na si lazima liwakilishe maoni ya USAID au Serikali ya Marekani”*

USAID
KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI

**USAID/TANZANIA UIMARISHAJI WA MIFUMO YA SEKTA ZA UMMA**

UHURU NA UMOJA

# Bodi ya Uhariri


## Mwenyekiti

*Mhandisi. Joseph M. Nyamhanga*
*Katibu Mkuu – Ofisi ya Rais, TAMISEMI*

## Wajumbe

*Erick Kitali – TAMISEMI*
*Rebecca Kwandu – TAMISEMI*
*Desderi Wengaa – PS3*

## Waandishi

*Atley Kuni - TAMISEMI*
*Albano Midelo– Manispaa ya Songea*
*Sekela Mwasubila– Halmashauri ya Mji Kondoa*

## Mhariri Mkuu

*Gladys Mkuchu– PS3*

## Wahariri

*Erick Kitali – TAMISEMI*
*Desderi Wengaa – PS3*
*Atley Kuni - TAMISEMI*
*Gladys Mkuchu – PS3*

## Msanifu Kurasa

*Jacqueline Sombe – PS3*



## Jarida hili hutolewa na:

*Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-TAMISEMI*
*S.L.P 1923*
*Dodoma-Tanzania*
*Simu: (+255) 26 -2321234*
*Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz*
*Tovuti: www.tamisemi.go.tz*
*Blogu: blog.tamisemi.go.tz*
*Facebook: Ofisi ya Rais – TAMISEMI*
*Instagram: ortamisemi*

## Ndani ya Jarida Hili:

**Tahariri……………………………………………………………………………………........uk 6**

**Teknolojia, Nguvu ya OR-TAMISEMI kuufikia Umma……………….……………..……....uk 7**

**Mitandao ya habari yaleta mapinduzi ya mawasiliano……………………..……......…....uk 8**

**Mifumo Imara Nguzo ya Utendaji kazi Halmashauri ………………………….…...….......uk 10**

**Zaidi ya Milioni 300 Zaokolewa Mikutano ya Masafa ………….……………………..........uk 11**

**Utenzi…………………………...…………………………………………….…….…….....uk 12**

## *TAHARIRI:*

# Tunaishi katika Karne ya Teknolojia ya Mawasiliano

Ukweli ni kwamba tunaishi katika karne ya mawasiliano. Watu wote imewapasa kuijua technolojia bila kuachwa nyuma na mabadiliko haya yanayokwenda sambamba na ukuaji wa uchumi katika dunia, ambao unahitaji watu wenye maarifa ya teknolojia ya mawasiliano.

Kila kukicha matumizi ya mikutano kwa njia ya masafa (*Video conference),* yanaongezaka kutokana na uhitaji wa sasa, watu kutoka sehemu tofauti za dunia wanaweza kuwasiliana kwa njia ya tekhnolojia bila ya kuonana ana kwa ana au kusafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine, mathalani kwa watoa huduma za afya wanaweza kutoa huduma hizo wakiwa mbali na mpewa huduma au watoa huduma ya elimu wanaweza kufanya hivyo.

Kwa upande wetu OR-TAMISEMI, *Video Conference* imeweza kuunganisha mikoa yote 26 ya Tanzania Bara katika huduma hii muhimu. Shabaha ni kuhakikisha ofisi inatumia vyema maendeleo haya ya teknolojia kama nyenzo muhimu ya mawasiliano na kuepusha baadhi madhara yanayoepukika.

Kupitia *Video Conference*, OR-TAMISEMI tumefanikiwa kuepusha madhara yanayoepukika katika barabara kwa watu kusafiri kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine, kupunguza gharama za fedha ambazo sasa zinaweza kuelekezwa katika matumizi mengine. *Video conference* imesaidia kuokoa muda mwingi uliokuwa unapotea barabara kwa watu kusafiri kwenda eneo la kikao ambapo muda huo unatumika kutoa huduma.

Kwakutambua umuhimu wa *Video Conference,* nitoe wito kwa viongozi ngazi za Mikoa na Halmashauri wanapotaka kuwasiliana wao kwa wao, yaani baina ya Mkoa mmoja na mwingine hawana haja yakusafiri tena wanaweza kufanya vikao vyao kwa njia ya video. Mathalani wana ajenda ya ujirani mwema kuhusiana na hali ya ulinzi na usalama, kilimo, uvuvi au ufugaji wanaweza kujadiliana kwa njia ya video conference.

Niwatakie usomaji mwema wa Jarida hili la Mifumo Yetu ambalo limeangazia vyema umuhimu wa *Video Conference* pamoja na Makala zingine zihusuzo umuhimu wa teknolojia katika maendeleo ya mwanachi.



**Mhandisi. Joseph M. Nyamhanga**

**Katibu Mkuu, OR -TAMISEMI**

## KUTOKA DODOMA

# Teknolojia, Nguvu ya OR-TAMISEMI kuufikia Umma

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) imetumika ipasavyo na kuifanya OR–TAMISEMI kuwa moja ya taasisi za umma nchini Tanzania ambazo zinatumia TEHAMA katika utoaji huduma na taarifa kwa wananchi kwa ufanisi na kwa gharama nafuu.

Matumizi haya ya teknolojia yanadhihirisha wazi kuwa ofisi hii inatekeleza Sera ya TEHAMA ya Mwaka 2016 inayosisitiza matumizi ya TEHAMA katika shughuli za Serikali ili kurahisisha utendaji kazi. Pia inaonesha haijabaki nyuma katika matumizi ya TEHAMA ambapo dunia nzima kwa sasa inashuhudia mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Kasi hii ya matumizi ya TEHAMA katika OR-TAMISEMI imechagizwa na jitihada za Wadau wa Maendeleo ambao wamejikita katika kuimarisha mifumo ya sekta za umma ikiwemo Afya, Elimu, Utawala na Miundombinu.

OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na wadau wake imefanya mapinduzi makubwa katika eneo la utoaji huduma na utawala. Jitihada hizi zimefanywa na zinaendelea kufanywa ili kuhakikisha Serikali za Mitaa na watumishi wake kwa jumla wanajengewa mifumo imara na uwezo ili kuboresha utendaji kazi kila siku.

Kwa jitihada hizo Mfumo wa Mipango, Bajeti na Utoaji wa Taarifa *(Planning and Reporting system-PlanRep),* umetengenezwa na wataalamu wa ndani na unatumika katika Halmashauri 185 zilizopo Tanzania Bara. Mfumo huu ni mkombozi wa shughuli za bajeti ambapo hapo awali Wizara na wadau wake walitumia takribani shilingi bilioni 8 ilhali sasa wanatumia bilioni 4 kila mwaka kwa shughuli za bajeti.

Aidha, katika kuhakikisha mfumo huu unakuwa endelevu, OR-TAMISEMI ilitengeneza mwongozo kwa njia ya video unaopatikana katika chaneli ya Youtube ya Wizara https://www.youtube.com/watch?v=JrQcKMstk18 ambapo watumishi wa umma wa Mikoa na Halmashauri zote wanaweza kusikiliza na kufuata maelekezo ya jinsi ya kutumia mfumo huo.

Uwepo wa video hiyo ya mafunzo ya mfumo wa PlanRep na mifumo mingine kama FFARS na EPICOR 10.2 kwenye akaunti ya YouTube ni ushahidi kwamba Wizara inatumia vema fursa za TEHAMA zilizopo kupitia Wadau




***Mkurugenzi wa TEHAMA Ofisi ya Rais TAMISEMI Erick Kitali akitoa mada kuhusu mifumo inayosimamiwa na Wizara hiyo katika mkutano mkuu wa 35 wa ALAT mwaka 2018 (Picha: OR TAMISEMI)***

hawa wa Maendeleo.

Katika hatua nyingine Mkurugenzi wa TEHAMA OR-TAMISEMI, Erick Kitali anasema kuwa idara yake ambayo ina jukumu la kusimamia masuala ya TEHAMA TAMISEMI inaendelea na jitihada za kuboresha mazingira ya upatikanaji wa huduma kwa umma na kwa wakati.

"Mwaka 2017 tulitengeneza tovuti kwa ushirikiano na eGA na PS3 na katika kipindi hicho Mikoa yote Tanzania Bara na Halmashuri zote 185 ziliwezeshwa kuwa na tovuti, Halikadhalika katika kipindi hiki cha miaka miwili tumeweza kutengeneza nyenzo ya ufatiliaji na uwekaji wa maudhui kwa lengo la kufanya usimamizi na ufuatiliaji wa tovuti hizo. Aidha, kwa kutumia nyenzo hiyo makao makuu wanaweza kupandisha tukio hilo mara moja na kuonekana katika tovuti zote 211 kwa wakati mmoja," alisema Kitali.

Nteghenjwa Hoseah, Afisa Habari kutoka OR-TAMISEMI anasema kutokana na ukuaji wa teknolojia shughuli za uhamasishaji kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa zimekuwa rahisi sana kwa kuwa unapandisha tangazo sehemu moja na linasambaa sehemu mbalimbali kwa muda mfupi.

"Vilevile katika ukurasa wetu wa jamii wa *Instagram* kabla ya kuanza hamasa ya shughuli za uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa mwaka huu wa 2019 tulikuwa na watu wanaotufatilia takribani 6400 lakini wakati wa zoezi la hamasa kwa mpiga kura idadi hiyo imeongezeka na kufikia watu elfu 32," anasema Nteghenjwa.

Nteghejwa anaongeza kuwa dawati la habari liko mstari wa mbele kupandisha na kuchapisha na kupeleka hewani taarifa mbalimbali ili kukidhi haja ya umma ya kupata habari kwa wakati.

OR-TAMISEMI, inatajwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 145 na 146 ambazo zinasisitiza kupeleka madaraka kwa wananchi na kuwahudumia. Hivyo jitihada hizi ni ishara tosha kwamba Wizara na wadau wake wamehakikisha kuwa wanazingatia takwa hili la kikatiba.

***Atley Kuni- OR TAMISEMI***

*KUTOKA MANISPAA YA SONGEA*

# Mitandao ya habari yaleta mapinduzi ya mawasiliano katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea

Mawasiliano kupitia mitandao ya habari ikiwemo tovuti na mitandao ya kijamii imeleta mapinduzi katika sekta ya habari na mawasiliano katika ngazi ya Halmashauri nchini.

Sekta hiyo inatoa mchango muhimu katika kuwezesha sekta nyingine za uchumi kwa kutoa miundombinu ya mawasiliano ya huduma ili kuruhusu mtiririko wa haraka wa habari, kubadilishana na kushirikishana taarifa baina ya Serikali na wananchi kwa ajili ya kuongeza ufanisi na kuimarisha utendaji wenye tija.

Halmashauri ya Manispaa ya Songea iliyopo mkoani Ruvuma ni moja ya Halmashauri nchini ambayo imepata mafanikio makubwa kupitia nguvu ya tovuti na mitandao ya kijamii ambayo imeunganishwa na tovuti ya Manispaa ya Songea.

Tovuti ya Manispaa ya Songea hadi kufikia Oktoba 30, 2019 ina watazamaji zaidi ya 16,000, TV ya mtandaoni ina watazamaji 977,367 na mitandao ya kijamii inatembelewa na idadi kubwa ya watu.

Mkuu wa Idara ya Utumishi katika Manispaa ya Songea Lewis Mnyambwa anasema tovuti ya Manispaa ya Songea imekuwa msaada mkubwa kwa kuwa imerahisisha mawasiliano kati ya watumishi na wananchi wa kawaida.

"Hivi sasa tukiwa na matangazo tunatumia tovuti, kwa mfano hivi karibuni majina ya walioteuliwa kuandikisha daftari la wapiga kura tuliweka kwenye tovuti na watumishi walipata taarifa kwa haraka,' anasema Mnyambwa.

Stani Kibiki ni Afisa Mtendaji wa Kata ya Mjimwema Manispaa ya Songea anasema tangu ilipoanzishwa tovuti ya Manispaa ya Songea mwaka 2017, imekuwa ni msaada mkubwa ambapo



***Wakazi wa Manispaa ya Songea wakiwa katika ubao wa matangazo ambao ulikuwa njia pekee iliyotumika kupata taarifa na matangazo kwa wananchi wa eneo hilo (Picha: Albano Midelo Manispaa ya Songea)***

amekuwa anapata taarifa mbalimbali zinazotokea katika Manispaa ya Songea, Wilaya, Mkoa na Taifa kwa ujumla.

Jane Shitindi ni Mchumi katika Manispaa ya Songea anasema Idara ya Uchumi na Mipango imekuwa inashirikiana na kitengo cha TEHAMA kuhakikisha miradi inayotekelezwa inatangazwa na kufahamika kwa wananchi.

"Miradi inatangazwa mara kwa mara kwenye tovuti na mitandao hali ambayo imesababisha wananchi wengi kutambua shughuli zinazofanywa na serikali katika Manispaa yetu," anasisitiza Shitindi.

Januari Antoni ni mkazi wa Mjini Songea anasema amekuwa anafuatilia habari mbalimbali zinazochapishwa katika tovuti na mitandao ya Manispaa ambapo amekuwa anafaidika na taarifa mbalimbali zikiwemo habari na matangazo mbalimbali yakiwemo na nafasi za kazi.

"Mimi kuna ndugu zangu wawili wamepata kazi baada ya kupata tangazo la kazi kupitia tovuti ya Manispaa ya Songea, pia kuna mambo mengi katika tovuti hii ambayo yanatoa taarifa na kuelimisha wananchi," anasisitiza Januari.

Mkuu wa Wilaya ya Songea Mhe.Pololet Mgema anasema tovuti ya Manispaa ya Songea imekuwa kiungo muhimu kati ya serikali na wananchi kwa sababu inatoa taarifa mbalimbali za serikali na kwenda kwa wananchi kupitia habari fupi, matangazo na video.

"Kila kitu ambacho tunafanya Serikalini unakikuta kwenye tovuti

***Inaendelea uk. 9***

*Inatoka uk. 8*

## ♦ *Mitandao ya Habari yaleta mapinduzi*

na mitandao yake, wananchi pia wanatoa maoni na viongozi tunatoa ufafanuzi kuhusu maoni yao, hii ni moja ya njia za kisasa ya kufikisha habari kwa haraka kwa wananchi," anasema Mgema.

Anasisitiza kuwa mitandao ya kihabari ni njia yenye gharama nafuu na rahisi kuwafikia watu wengi kwa muda mfupi.

Profesa Joseph Mbele ni Mtanzania ambaye anaishi nchini Marekani, mzaliwa wa Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma, anasema tovuti ya Manispaa ya Songea imemfanya kujiona kama yupo nyumbani kwa sababu anapata taarifa zote za mkoani Ruvuma.

***Profesa Mbele ambaye ni Mhadhiri nchini Marekani, anasema amekuwa anafuatilia tovuti ya Manispaa na mitandao ambayo inatoa taarifa mara kwa mara kuhusu Mkoa wa Ruvuma hivyo anajisikia kama yupo nyumbani.***

Kwa ujumla tovuti ya Manispaa ya Songea imeleta mapinduzi makubwa katika TEHAMA sio kwa Manispaa ya Songea tu bali Wilaya ya Songea, Mkoa wa Ruvuma na Taifa kwa ujumla.

Kuanzishwa kwa tovuti za Halmashauri nchini Tanzania kumewezesha ukuaji wa haraka wa huduma za mawasiliano. Huduma za TEHAMA hivi sasa zinafika kwenye baadhi ya maeneo ya vijijini na maeneo mengi mijini.

Mwenendo unaonesha kuwa viongozi wa serikali na siasa katika Mji wa Songea, hivi sasa wanatumia mitandao ya kijamii katika mijadala na utoaji wa taarifa mbalimbali kwa wananchi.

Tito Sovera ni Mtangazaji wa Key FM redio ambayo inarusha matangazo kutoka Mjini Songea anasema kuwa utumiaji wa mitandao ya kijamii na tovuti ya Manispaa ya Songea umesababisha kituo chao kupata taarifa kwa haraka na kuongeza nguvu ya habari katika redio yao.

Sovera anasema kila siku wamekuwa wanaingia kwenye tovuti ya Manispaa ya Songea na kupakua habari mpya ambazo zinatumika kwenye redio. Hivyo tovuti zimesaidia kuweza kupata taarifa kwa haraka na sahihi.

Julius Konala ni Mwandishi wa habari wa kujitegemea anasema tangu kuanzishwa na tovuti ya Manispaa ya Songea amekuwa anaingia na kupakua habari ambazo huwa anazituma kwenye magazeti mbalimbali hivyo kurahisisha ukusanyaji na usambazaji wa habari.


Christopher Ngonyani ni Afisa Uchaguzi wa Manispaa ya Songea anasema katika mchakato mzima wa kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambao unatarajia kufanyika nchini kote tarehe 24 Novemba 2019, tovuti ya Manispaa ya Songea na mitandao yake imekuwa msaada mkubwa wa kutangaza kila hatua.

"Ukingia kwenye tovuti ya Manispaa ya Songea utakuta matangazo mbalimbali ya uchaguzi wa serikali za mitaa ambayo pia yapo kwenye, mitandao ya kijamii ya Youtube na facebook. Kwa kweli mitandao imeleta mapinduzi makubwa katika mawasiliano," anasisitiza Ngonyani.

Nchi nyingi zilizoendelea na zinazoendelea zimepata mafanikio makubwa katika sekta mbalimbali kutokana na kutumia TEHAMA katika simu, tovuti na mitandao ya kijamii kama Blogu, Facebook, Twitter, Youtube na mitandao mingine ya kihabari .

Tovuti ya Manispaa ya Songea inapatikana kupitia http://www.songeamc.go.tz/

***Albano Midelo– MANISPAA YA SONGEA***



*Mchumi katika Manispaa ya Songea Oscar Ngalomba akiperuzi taarifa mbalimbali kwenye tovuti ya Manispaa hiyo ambapo matangazo na taarifa zote zinaweka katika tovuti hiyo (Picha: Albano Midelo, Manispaa ya Songea)*

## KUTOKA KONDOA

# Mifumo Imara Nguzo ya Utendaji kazi Halmashauri

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa Msoleni Dakawa ameishukuru OR-TAMISEMI kwa kuanzisha mifumo mbalimbali na kuwaomba waendelee kutengeneza mifumo mingine kwani inaokoa muda wa kuwahudumia wananchi na kupunguza gharama za uendeshaji wa Halmashauri hali inayopelekea fedha zilizokuwa zinatumika kuwalipa posho watumishi kutumika katika shughuli za maendeleo.




Amesema hayo akizungumzia kuhusu umuhimu na faida za mifumo mbalimbali ya serikali iliyounganishwa taarifa zake na mitandao ya kijamii katika kurahisisha huduma mbalimbali za serikali.

Anaeleza kuwa awali Halmashauri ilikuwa ikitumia zaidi ya shilingi milioni 50 kama posho za wataalam kutoka Idara mbalimbali waliokuwa wakisafiri kwaajili ya maandalizi ya bajeti sehemu nyingine kwa siku zisizopungua 35 hadi 45 kwa kila mwaka, fedha ambazo zingeweza kutumika katika kutoa huduma kwa wananchi lakini toka uanzishwe mfumo wa Mipango na Bajeti (PlanRep) kila kitu kinafanyika eneo la kituo.

"Sambamba na mfumo PlanRep vilevile kabla ya uwepo wa mfumo wa Taarifa wa Kiutumishi na Mishahara (LAWSON) ilimlazimu Afisa Utumishi kusafiri na nyaraka za watumishi hadi wizarani ili zifanyiwe kazi jambo ambalo lilikuwa likileta malalamiko mengi sana kutoka kwa watumishi kwa kucheleweshewa haki zao. Lakini mfumo huo ulipoanzishwa asilimia 90 ya malalamiko yamepungua kwani kila kitu kinafanywa katika halmashauri kwa kuweka viambata vya taarifa za mhusika katika mfumo na kufika wizarani kwa wakati," anasema Dakawa.

> ***"Matokeo ya matumizi sahihi ya tovuti yetu ya Kondoa Mji, ndio chachu ya ujio wa wanakondoa waishio nchini Marekani kutembelea na kisha kuunga mkono jitihada za Maendeleo zinazofanywa na wananchi wa Kondoa Mji kwa kushiriki kwenye zoezi la Kliniki ya Macho kwa mustakabali wa Afya za Watanzania wa Kondoa na Tanzania kwa ujumla." Dkt. Dorothy Gwajima Naibu Katibu Mkuu OR-TAMISEMI***

"Mifumo mingi imeturahisishia kazi katika idara zote ikiwemo kuondoa kabisa foleni za malipo ofisi ya fedha kwani kwa sasa wananchi wanapewa namba maalum na kwenda kulipia benki. Vilevile mfumo wa BEMIS upande wa elimu umesaidia kupata takwimu mbalimbali za kielimu, sambamba na mfumo wa uendeshaji shughuli za Afya (Government of Tanzania Health Operation Management Information Systerm – GOTHOMIS). Hata hivyo uwepo wa mitandao ya kijamii pia umesaidia sana katika kufikisha taarifa mbalimbali kwa wananchi kwa muda mfupi na kupata mrejesho wa masuala mbalimbali kutoka kwa wananchi na kufanyiwa kazi ambapo hapo awali ilikuwa ni vigumu sana kupata taarifa hizo na kupelekea baadhi ya wananchi kuandamana sababu walikuwa wakikosa sehemu ya kusemea.

Mwaka 2017 Halmashauri ilianzisha ukurasa wa *Facebook* ujulikanao kama KONDOA TC na ina jumla ya wafuatiliaji zaidi ya 900 ambao hupata taarifa mbalimbali za Halmashauri kwa wakati huohuo na wao huchangia kwa kutoa maoni yao katika ukurasa huo na ofisi huyachukua na kuyafanyia kazi lakini pia kurasa zingine za ofisi ni *Instagram* (kondoatc2015), *Youtube* (KondoaTC) na Twitter (Kondoa TC)

Egid Mhema ni mmoja ya watu waliochangia na maoni yake katika kurasa zetu ulisomeka "Hongereni sana kilakitu kinawezekana kwa watu wenye nia moja, ushirikiano, nidhamu ya utekelezaji na usimamizi. *Keep it up*".


Aidha kwa uwepo wa tovuti ya Halmashauri ya Mji kondoa www.kondoatc.go.tz tovuti iliyoanzishwa na OR-TAMISEMI, Halmashauri ya Mji inajivunia sana kwani Februari 2018 iliwekwa taarifa ya Mheshimiwa Mbunge kutoa msaada wa miwani kwa wananchi na kusambaa kwa wananchi wengi ndani na nje ya nchi na kuwagusa wananchi wa Kondoa waishio nchini Marekani na kuahidi kuja kutoa huduma ya matibabu bure kwa wananchi wa Kondoa huduma ilifanyika Septemba 2018 na mgeni rasmi alikuwa Dkt. Doroth Gwajima ambaye kwasasa ni Naibu Katibu Mkuu OR-TAMISEMI.

***Sekela Mwasubila– Kondoa Mji***

*KUTOKA DODOMA*

# Gharama na Muda Vyaokolewa Mikutano ya Masafa

Fedha na muda vimekuwa vikiokolewa kila mwaka na kuelekezwa kwenye matumizi mengine ya Serikali kutokana na OR-TAMISEMI kufanya mikutano yake kwa kwa njia ya masafa kupitia mitandao, *Video Conference* baina yake na wadau wake yaani Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine.



***Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI Mhe. Selemani Jafo pamoja na viongozi wengine wa Wizara hiyo akiwa katika mkutano wa masafa na Wakuu wa Mikoa yote nchini (Picha: OR TAMISEMI )***

Kwa mujibu wa taarifa ya uendeshaji wa vikao hivyo iliyotolewa na OR-TAMISEMI kupitia idara ya TEHAMA, inaonesha kuwa uwepo wa mfumo huo katika wakati wa sasa umekuwa mkombozi na umeongeza tija, ufanisi na kuepusha baadhi ya mambo ikiwepo kupoteza muda mwingi njiani kusafiri kwenda kwenye vikao.

Mkurugenzi wa TEHAMA OR-TAMISEMI, Erick Kitali anasema kuwa, "kabla yakufungwa kwa mfumo ililazimu viongozi na wataalam kutoka ngazi za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kusafiri kutoka eneo moja la nchi hadi lingine kutegemea mkutano umeitishwa eneo gani lakini tangu wamefunga mfumo kwenye mikoa 26 nchi nzima, pamoja na OR-TAMISEMI Makao Makuu, imerahisisha sana na kuokoa muda."

Kitali anaongeza kwamba, mbali na gharama hizo za fedha, lakini pia muda mwingi ulitumika kusafiri kwenda kwenye vikao kwa hivi sasa haupo kwani kwakutumia mfumo imesaidia viongozi na watendaji kuendelea na majukumu yao mengine katika maeneo yao ya kazi.

"Mfano rahisi ni mikutano ya hivi karibuni ambapo Waziri Mkuu Mheshimiwa Kasimu Majaliwa Majaliwa, aliendesha Mkutano na Viongozi wa Mikoa inayolima zao la Korosho sambamba na Mkutano baina ya Naibu Katibu anayeshughulikia Afya OR-TAMISEMI Dkt. Dorothy Gwajima na Waganga Wakuu wa Mikoa, endapo tusingetumia Video Conference ingelazimu wahusika kusafiri ambapo wangetumia magari wangejilipa posho na wangetumia muda wa siku mbili za kusafiri na siku moja nje ya kituo," anasisitiza Kitali.

Kwa upande wake Mtaalam wa TEHAMA anaye simamia mfumo huo Hamimu Malowa, anasema, "Lengo la kuanzisha mfumo wa *Video Conference* tangu mwaka 2013 katika ofisi za Serikali ni kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya watumishi Serikalini."

"Kwa kutumia huduma hii, viongozi na watendaji na wataalam wameweza kufanya kazi zao kwa kushirikiana na kuwasiliana na wadau wengine wakiwa katika maeneo yao ya kazi bila ya kulazimika kusafiri kutoka sehemu zao za kazi na kwenda sehemu nyingine na hivyo kupunguza hatari ya muda mwingi unaotumika katika vyombo vya usafiri na kuimarisha mawasiliano serikalini sambamba na huhamasisha matumizi ya Serikali mtandao na kupunguza urasimu. Mfumo huu pia umesaidia kuharakisha utoaji wa maamuzi na utekelezaji wa majukumu ndani ya Serikali na kwa wananchi," anaongeza Malowa.

Wazo la kuwa na miundominu hiyo, ilitokana na gharama zilizokuwa zikijitokeza kutokana na wingi wa vikao vilivyokuwa vikifanyika kati ya OR-TAMISEMI na Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala Mikoa, Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine.

OR-TAMISEMI, kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi walifunga mfumo wa vifaa vya kuendeshea mikutano kwa njia ya masafa katika mwaka wa fedha 2012/13 ambapo OR-TAMISEMI na Ofisi za Mikoa zilifungiwa vifaa hivyo kwa ajili kurahisisha zoezi la kufanya mikutano.

Katika awamu ya kwanza Mikoa 22 ya Tanzania Bara ilinufaika na mradi huo na katika mwaka wa fedha 2018/19 Mikoa minne ya Songwe, Geita, Njombe na Simiyu ambayo ilikuwa bado nayo ilifungiwa vifaa vya mikutano na kufanya jumla ya Mikoa 26 ya Tanzania bara kuunganishwa na vifaa vya kuendeshea mikutano.

***Atley Kuni– OR TAMISEMI***

# UTENZI

## Mifumo Kushamiri, Manufaa kwa Wananchi

Ukweli umedhihiri, Mifumo imedhibiti,
Mifumo hii mahiri, Wajanja kuwadhibiti,
Mapato mengi halali, Matokeo Madhubuti,
**Mifumo Kushamiri, Manufaa kwa wananchi**

Uko ule wa mapato, Na makusanyo kwakweli,
Unakusanya za sato, Hata zile basikeli,
Na Wilaya zipo Moto, Malipo yote halali.
**Mifumo Kushamiri, Manufaa kwa wananchi**

Mipango sasa wapanga, Ndugu zangu kule Nyasa,
Na Gharama mepunguza, Kusafiri hasa hasa,
Wapange kule Muheza, Tamisemi tafikisha,
**Mifumo Kushamiri, Manufaa kwa wananchi**

Mfumo mwingine ni FFARS, Watumika vituoni,
Umeweka Mambo wazi, Wakora hatuwaoni,
Wafanyapo Matumizi, Hesabu zake baini,
**Mifumo Kushamiri, Manufaa kwa wananchi**

Kazi hii sio ndogo, Wajuzi wetu wa ndani,
Hawataki hali Jojo, Mambo yote ushindani,
Subuhi hadi jogoo, 'Code' wapiga ndani,
**Mifumo Kushamiri, Manufaa kwa wananchi**

Kitali kinara wao, Kiongozi motomoto,
Kufatilia ni kwao, Uzalendo kwenye roho,
Hakeshi kucheza bao, Ndotoze kwenye mifumo,
**Mifumo Kushamiri, Manufaa kwa wananchi**

Tunayo mifumo mingi, BEMIS niwa Skuli,
Unazo Takwimu nyingi, Toka zile za awali
Madawati ya Msingi, Wote tumeukubali,
**Mifumo Kushamiri, Manufaa kwa wananchi**

Palipo Hospitali, Wameundiwa mfumo,
Taratibu kila hali, Zahanati zikiwemo,
Hospitali Mbarali, na Kigoma wakiwemo
**Mifumo Kushamiri, Manufaa kwa wananchi**

Mbele ninaendelea, Kuwatajia Mifumo,
Kishkwambi chatumika, Ni SIS wake Mfumo,
Wamepewa Watandika, Pia Shuleni Nyashimo,
**Mifumo Kushamiri, Manufaa kwa wananchi**

Alisimama Waziri, Mifumo kusimulia,
Makusanyo medhihiri, Silimia mekulia,
Juhudi hizi ambari, Mifumo kushikilia.
**Mifumo Kushamiri, Manufaa kwa wananchi**

Faidaze niyakini, Uchumi kuupaisha,
Huduma za kijamii, zote hizi meboresha,
Ni Udhibiti Jamani, Mifumo inatukosha,
**Mifumo Kushamiri, Manufaa kwa wananchi**

Uvivu jama tuache, Dunia inakimbia,
Na TEHAMA situache, Wenzangu nawaambia,
Haki vile tusikache, Wenzetu wanakimbia,
**Mifumo Kushamiri, Manufaa kwa wananchi**

Kadi tama nimefika, TEHAMA nimekwambia,
Dunia inasifika, Malawi pia Zambia,
Ni dhambi kuachwa nyuma, Mwishowe nimepambia,
**Mifumo Kushamiri, Manufaa kwa wananchi**

Niweke wazi tasisi, Nawakala ya Serikali,
Yupo eGA ni Mwasisi, Hazina sio wakali,
Malipo yote kimtandao, GePG Twaikubali,
**Mfumo kushamiri, Manufaa kwa wananchi**

Asante kufatilia, ujumbe umetukuka
Atley mwana wa Kuni, Malenga nimetumika,
Mifumo wote tupende, Muhimu ikitumika
**Mifumo Kushamiri, Manufaa kwa wananchi,**

***Atley Kuni– OR TAMISEMI***